



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA MBOZI

Simu . Na. 025 – 2580272
Nukushi Na. 025 – 2580044
Barua pepe.ded@mbozidc.go.tz

S. L. P. 3,
MBOZI.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.A.10/MDC/31/2

26/05/2022.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi anawatangazia nafasi za kazi za Katibu Mahsusi Daraja la III, Mtunza Kumbukumbu Msaidizi Daraja la II na Mhudumu wa Jikoni. Nafasi hizi za ajira zinatokana na kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa barua Kumb.Na.FA.17/228/01/9 ya tarehe 13 Mei, 2022.

1.0. **MHUDUMU WA JIKONI (NAFASI 1)**

1.1. **MAJUKUMU YA KAZI**

- (a) Kusafisha vyombo vya kupikia
- (b) Kusafisha vyombo vya kulia chakula
- (c) Kuwatayarishia wapishi/waandazi wa vifaa vya kazi
- (d) Kusafisha maeneo ya kupikia
- (e) Kuwasaidia waandazi wa wapishi
- (f) Kusafisha meza itumiwayo kwa kulia chakula

1.2. **SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe amehitimu kidato cha nne mwenye cheti cha mafunzo ya uhudumu jikoni kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali

1.3. **MSHAHARA**

- Mshahara atalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali TGOS A

2.0. KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III (NAFASI 1)

2.1. MAJUKUMU YA KAZI

- (a) Kuchapa barua na nyaraka za kawaida
- (b) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- (c) Kusaidia kutunza taarifa, kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anapofanyia kazi na kumtaarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- (d) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.
- (e) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi wake.
- (f) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maafisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

2.2. SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha nne au sita
- Awe amehudhuria mafunzo ya Uhadhili na kufaulu.
- Awe amefaulu Hati Mkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika na awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti.

2.3. MSHAHARA

- Mshahara atalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali TGS B1

3.0. MTUNZA KUMBUKUMBU MSAIDIZI DARAJA LA II (NAFASI 1)

3.1. MAJUKUMU YA KAZI.

- (a) Kutafuta kumbukumbu, nyaraka, mafaili yanayohitajiwa na wasomaji.
- (b) Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka
- (c) Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka n.k) katika mafaili.
- (d) Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka taasisi za Serikali.
- (e) Kuweka na kupanga kumbukumbu katika chumba cha kuhifadhia kumbukumbu.

3.2. SIFA ZA MWOMBAJI

- Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha nne, sita wenye cheti cha Utunzaji Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

3.3. MSHAHARA

- Mshahara atalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali TGS B1

4.0. MASHARTI YA JUMLA

- Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na wasiozidi miaka 45.
- Mwombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni (Passport size).
- Waombaji wawasilishe maelezo binafsi yanayojitosheleza yenye anuani za namba za simu.
- Waombaji wote waambatanishe nakala ya vyeti halisi vya masomo na taaluma (NTA Level 5) na Transcript ya cheti cha taaluma, cheti cha kuzaliwa. Mwombaji atakayewasilisha "Result" "statement of result", "provisional result" au "Transcript" bila nakala halisi ya cheti cha taaluma maombi yake hayatakubaliwa.
- Kwa waliosoma nje ya nchi Elimu ya Kidato cha nne na Kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- Waombaji wawasilishe nakala ya kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
- Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatahughulikiwa.
- Maombi yaandikwe kwa mkono na yatumwe kwa njia ya Posta kupitia anuani iliyotajwa hapo chini.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09/06/2022.

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI,
S.L.P 3,
MBOZI.**

Imetolewa na.



Abdallah H. Nandonde
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MBOZI.